**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**
**2020 - 2025**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Zubeir Ali Maulid | - | SPIKA |
| 2. | Mhe. Mgeni Hassan Juma | - | Naibu Spika/Nafasi za Wanawake |
| 3. | Mhe. Hemed Suleiman Abdulla wa | - | MBM/Makamu wa Pili Rais//Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Uteuzi wa Rais |
| 4. | Mhe. Abdalla Hussein Kombo | - | Jimbo la Mkoani |
| 5. | Mhe. Abdalla Abass Wadi | - | Jimbo la Nungwi |
| 6. | Mhe. Ali Abdulghulam Hussein | - | Jimbo la Jang'ombe |
| 7. | Mhe. Ali Suleiman Ameir | - | Jimbo la Pangawe |
| 8. | Mhe. Ameir Abdalla Ameir | - | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 9. | Mhe. Anna Athanas Paul | - | Uteuzi wa Rais |
| 10. | Mhe. Asha Abdalla Mussa | - | Jimbo la Mahonda |
| 11. | Mhe. Aza Januar Joseph | - | Nafasi za Wanawake |
| 12. | Mhe. Bahati Khamis Kombo | - | Jimbo la Chambani |
| 13. | Mhe. Bakari Hamad Bakari | - | Jimbo la Wawi |
| 14. | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | - | Nafas iza Wanawake |
| 15. | Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed (Mandoba) | | Nafasi za Wanawake |
| 16. | Mhe. Habibu Ali Muhamed | - | Jimbo la Mtambwe |
| 17. | Mhe. Haji Omar Kheri | - | Jimbo la Tumbatu |
| 18. | Mhe. Haji Shaaban Waziri | - | Jimbo la Uzini |
| 19. | Mhe. Hamza Hassan Juma | - | Jimbo la Kwamtipura |
| 20. | Mhe. Haroun Ali Suleiman | - | Jimbo la Makunduchi |
| 21. | Mhe. Harusi Said Suleiman | - | Jimbo la Wete |
| 22. | Mhe. Hassan Hamad Omar | - | Jimbo la Kojani |
| 23. | Mhe. Hassan Khamis Hafidh | - | Jimbo la Welezo |
| 24. | Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir | - | Nafasi za Wanawake |
| 25. | Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | - | Jimbo la Mtoni |
| 26. | Mhe. Jamal Kassim Ali | - | Jimbo la Magomeni |
| 27. | Mhe. Juma Makungu Juma | - | Jimbo la Kijini |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 28. Mhe. | Juma Ali Khatib | - | Uteuzi wa Rais |
| 29. Mhe. | Dkt Khalid Salum Mohamed | - | Jimbo la Donge |
| 30. Mhe. | Issa Haji Ussi Gavu | - | Jimbo la Chwaka |
| 31. Mhe. | Kombo Mwinyi Shehe | - | Jimbo la Wingwi |
| 32. Mhe. | Lela Mohamed Mussa | - | Nafasi za Wanawake |
| 33. Mhe. | Machano Othman Said | - | Jimbo la Mfenesini |
| 34. Mhe. | Maryam Thani Juma | - | Jimbo la Gando |
| 35. Mhe. | Masoud Ali Mohammed | - | Jimbo la Ole |
| 36. Mhe. | Mihayo Juma Suleiman | - | Jimbo la Mwera |
| 37. Mhe. | Miraji Khamis Mussa | - | Jimbo la Chumbuni |
| 38. Mhe. | Mohamed Mgaza Jecha | - | Jimbo la Mtambile |
| 39. Mhe. | Mohamed Ahmada Salum | - | Jimbo la Malindi |
| 40. Mhe. | Mudrik Ramadhan Suleiman | - | Jimbo la Bububu |
| 41. Mhe. | Mtumwa Peya Yussuf | - | Jimbo la Bubwini |
| 42. Mhe. | Mussa Foum Mussa | - | Jimbo la Kiwani |
| 43. Mhe. | Mwanaasha Khamis Juma | - | Jimbo la Dimani |
| 44. Mhe. | Mwanaidi Kassim Mussa | - | Nafasi za Wanawake |
| 45. Mhe. | Mwantatu Mbarak Khamis | - | Nafasi za Wanawake |
| 46. Mhe. | Mwanajuma Kassim Makame | - | Nafasi za Wanawake |
| 47. Mhe. | Dkt. Mwinyi Talib Haji | - | Mwanasheria Mkuu |
| 48. Mhe. | Nadir Abdullatif Yussuf | - | Jimbo la Chaani |
| 49. Mhe. | Nassor Salim Ali | - | Jimbo la Kikwajuni |
| 50. Mhe. | Panya Ali Abdall | - | Nafasi za Wanawake |
| 51. Mhe. | Rahma Kassim Ali | - | Nafasi za Wanawake |
| 52. Mhe. | Riziki Pembe Juma | - | Nafasi za Wanawake |
| 53. Mhe. | Rukia Omar Ramadhan | - | Jimbo la Amani |
| 54. Mhe. | Saada Ramadhan Mwendwa | - | Nafas iza Wanawake |
| 55. Mhe. | Dkt. Saada Mkuya Salum | - | Uteuzi wa Rais |
| 56. Mhe. | Saidi Saleh Salim | - | Jimbo la Tumbe |
| 57. 5Mhe. | Sabiha Fil fil Thani | - | Nafasi za Wanawake |
| 58. Mhe. | Salha Mohamed Mwinjuma | - | Nafasi za Wanawake |
| 59. Mhe. | Salma Mussa Bilal | - | Nafasi za Wanawake |
| 60. Mhe. | Simai Mohammed Said | - | Jimbo la Tunguu |
| 61. Mhe. | Soud Nahoda Hassan | - | Jimbo la Paje |
| 62. Mhe. | Suleiman Masoud Makame | - | Jimbo la Chonga |
| 63. Mhe. | Suleiman Makame Ali | - | Jimbo la Ziwani |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 64. Mhe. | Suleima Haroub Suleiman Samaki | - | Jimbo la Kiembe |
| 65. Mhe. | Sulubu Kidongo Amour | - | Jimbo la Mkwajuni |
| 66. Mhe. | Shadya Mohamed Suleiman | - | Nafasi za Wanawake |
| 67. Mhe. | Shaaban Ali Othman | - | Jimbo la Mpendae |
| 68. Mhe. | Shamata Shaame Khamis | - | Jimbo la Micheweni |
| 69. Mhe. | Shaib Hassan Kaduara | - | Jimbo la Chake Chake |
| 70. Mhe. | Tabia Maulid Mwita | - | Uteuzi wa Rais |
| 71. Mhe. | Yahya Rashid Abdulla | - | Jimbo la Kwahani |
| 72. Mhe. | Yussuf Hassan Iddi | - | Jimbo la Fuoni |
| 73. Mhe. | Zaina Abdalla Salum | - | Nafasi za Wanawake |
| 74. Mhe. | Zawadi Amur Hassan | - | Jimbo la Konde |

**Ndg. Raya Issa Msellem - Katibu**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 11 Novemba, 2020**

*(Kikao kilianza saa 8:00 mchana)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua*

**TAARIFA YA SPIKA**

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuwapa taarifa rasmi kuwa Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Mjumbe Mwakilishi Mteule wa Jimbo la Pandani amefariki dunia usiku wa kuamkia leo Jumatano tarehe 11 Novemba, 2020 hapa Unguja. Afisi yangu na Baraza la Wawakilishi kwa ujumla tumepokea kwa huzuni kubwa taarifa za kifo hicho. Mhe. Abubakary alikuwa ni miongoni mwa wajumbe ambao hawakuwahi kuapishwa kiapo cha uaminifu cha kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Pandani na tulikuwa tukitarajia angeapishwa kiapo hicho katika siku za usoni. Kwa msingi huo bado alikuwa Mjumbe Mwakilishi Mteule kwa kuzingatia kuwa alikuwa bado hajaapishwa kiapo hicho.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary wengi wetu tumefanya naye kazi akiwa mjumbe mwenzetu wa Baraza la Wawakilishi katika awamu mbali mbali na pia tumefanya naye kazi katika ngazi mbali mbali. Katika awamu ya saba ya uongozi wa nchi yetu, aliitumikia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar akiwa kama Waziri wa Katiba na Sheria.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa niaba ya Baraza la Wawakilishi, tunawapa pole sana familia yake kwa kuondokewa na mpendwa wao. Aidha, tunawapa pole sana ndugu, jamaa na marafiki zake pamoja na chama chake kwa msiba huo. Kwa umuhimu wa kipekee, nawapa pole sana wananchi wa jimbo la Pandani kwa kuondokewa na kiongozi wao wa kuwawakilisha katika chombo chetu hiki cha uwakilishi wa wananchi ambapo kwa sasa hawatakuwa na uwakilishi kutokana na kiti hicho kuwa wazi kufuatia kifo hicho. Wote hao tunawaombea Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira katika wakati huu mgumu wa kuondokewa na mpendwa wao. Baraza la Wawakilishi litawakilishwa na baadhi ya viongozi katika msiba huo, ili kuungana na wanafamilia, ndugu, jamaa na marafiki katika kumstiri mwenzetu.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu amsamehe madhambi yake, mwenzetu Mhe. Abubakar Khamis Bakary na amjaalie pepo. *Innalillahi Wainna Ilayhi Rajiun.* Sasa Waheshimiwa Wajumbe naomba tusimame kwa muda wa dakika moja ili tumuombee mwenzetu dua kila mmoja kwa nafsi yake.

*(Hapa Waheshimiwa Wajumbe walisimama kwa dakika moja*
*ili kumuombea dua Marehemu Mhe. Abubakar Khamis Bakary)*

**Mhe. Spika:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe tunaweza kukaa.

Waheshimiwa Wajumbe, *order paper* kama kama tulizonazo mbele yetu, shughuli inayofuata ni Hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kwa hivi sasa Waheshimiwa Wajumbe, nitasitisha kidogo shughuli hizi ili baadae nitoke kwenda kumpokea Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na baadae kurudi naye kwa ajili ya kuja kukamilisha otoaji wa hotuba yake katika kukamilisha shughuli zetu hizi za Baraza la Wawakilishi.

Kwa msingi huo Waheshimiwa Wajumbe, ninawaomba waheshimiwa mbaki katika hali ya utulivu humu ndani, wakati mimi na baadhi ya watendaji tukiwa tunafanya hiyo kazi ya kuja kumsindikiza Mhe. Rais.

Jambo jengine Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijatoka ni kwamba leo mara baada ya hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tutaakhirisha kikao yaani mkutano huu utakuwa umekamilika, tumemaliza huu mkutano baada ya hiyo hotuba.

Lakini nimependekeza mmoja wenu mara baada ya neno la shukurani ambalo atalitoa Spika, baada ya kukamilika kwa hotuba ya Mhe. Rais, atoe hoja ya kuomba kwamba hotuba ile ijadiliwe. Sasa baada ya hapo nitawahoji na baada ya kukamilika tutatoa muongozo namna gani tutafanya hilo suala la kutoa hoja.

Kwa hivyo, jambo hilo litafanyika mara baada ya Mhe. Rais kutoa hotuba yake na mara baada ya Spika, kutoa neno lake la shukurani ndipo itakapotoka hiyo hoja. Kwa hivi sasa naomba Waheshimiwa Wajumbe tuendelee kukaa kwa utulivu, ili sasa niweze kwenda nje kwa ajili ya maandalizi ya kumpokea Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Kwa makofi hayo sasa, naomba nisitishe shughuli za Baraza mpaka hapo baadae kidogo, lakini nawaomba Waheshimiwa Wajumbe, mbaki humu ukumbini. Ahsanteni sana.

*(Saa 8:08 mchana Baraza liliakhirishwa kwa muda mchache kwa ajili ya Mhe. Spika kwenda kumpokea Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi)*

*(Saa 9:00 mchana Baraza lilirudia)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tafadhali sasa tunaweza tukakaa Waheshimiwa, tukaeni.

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi karibu sana katika Baraza la Wawakilishi, na kwa mujibu wa katiba wewe ni sehemu ya hili Baraza na shughuli tuliyonayo hapa ni ya hotuba yako. Lakini sasa kabla sijakukaribisha Mhe. Rais naomba ruhusa yako nitambue baadhi ya wageni ambao wamekuja kwa ajili ya kujumuika na wewe wakati ukitoa hotuba yako.

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wageni wetu wa leo ni viongozi, makundi tofauti. Kwanza ni Viongozi wa Kitaifa naomba niwatambue kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Omar Othman Makungu, Jaji Mkuu wa Zanzibar pamoja nae yuko na Mhe. Martin Mgoga - Spika wa Bunge la Afrika ya Mashariki *(EALA)*;
2. Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Rais Mstaafu wa Zanzibar;
3. Mhe. Amani Abeid Karume, Rais Mstaafu wa Zanzibar;

4. Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais Mstaafu wa Zanzibar. Mhe. Rais makofi hayo ni ya ushuhuda wa kazi nzuri ambayo umeifanya Mhe. Rais Mstaafu; *(Makofi)*
5. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais Mstaafu;
6. Mhe. Pandu Ameir Kificho, Spika Mstaafu wa Baraza la Wawakilishi karibu sana mzee wetu;
7. Mhe. Ali Abdulla Ali, Naibu Spika Mstaafu wa Baraza la Wawakilishi;
8. Mhe. Hassan Khatib Hassan, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi;
9. Ndg. Abdulhamid Yahya Mzee, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi;
10. Ndg. Saleh Kinana, Meya wa Jiji la Zanzibar.

Pamoja na hao, wageni wetu wengine ni wake wa Viongozi wa Kitaifa nao ni:-

Mhe. Mama Sharifa Hemed Suleiman, Mke wa Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar;

1. Mhe. Mama Siti Mwinyi, Mke wa Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
2. Mhe. Mama Shadya Karume, Mke wa Rais Mstaafu wa Zanzibar;
3. Mhe. Mama Mwanamwema, Mke wa Rais Mstaafu wa Zanzibar;

Mhe. Mama Asha Balozi, Mke wa Makamu wa Pili wa Rais Mstaafu wa Zanzibar;

Mhe. Mama Fatma Abdulla Mzee pamoja na Mhe. Mama Warda Haji Mwadini, hawa ni wake wa Spika wa Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Rais wa Zanzibar wapo Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa ambao wamefika hapa nao ni kama ifuatavyo:-

1. Balozi Mdogo wa Msumbiji;
2. Balozi Mdogo wa Oman;
3. Balozi Mdogo wa India;
4. Mwakilishi wa Ubalozi Mdogo wa China;
5. Mwakilishi wa *UNDP;*
6. Mwakilishi wa *WHO;*
7. Mwakilishi wa *IOM;*
8. Mwakilishi wa *UNAIDS;*
9. Mwakilishi wa *UNESCO;*
10. Mwakilishi wa *UNFP;*
11. Mwakilishi wa *UNICEF;*
12. Mwakilishi wa *UNRCO;*
13. Balozi wa Heshima wa Italy;
14. Balozi wa Heshima wa Brazil;

Pia wapo Wakuu wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama nao ni kama hivi ifuatavyo:-

1. Kamanda wa Jeshi (NYUKI BRIG.) Zanzibar;
2. Kamishna wa Polisi wa Zanzibar;
3. Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar;
4. Naibu Mkurugenzi Mkuu Usalama wa Taifa Zanzibar;
5. Kamanda wa KMKM Zanzibar;

6. Mkuu wa JKU Zanzibar;
7. Kamanda wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar;
8. Kamanda wa Kikosi cha Valantia Zanzibar;
9. Kamanda wa Zimamoto na Uokozi Zanzibar.

Pia wapo wageni kutoka familia ya Mhe. Rais wa Zanzibar naomba wasimame kwa pamoja.

Vile vile, wapo Wakuu wa Mikoa na Wilaya nao ni kama ifuatavyo:-

1. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja;
2. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja;
3. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba;
4. Mkuu wa Wilaya ya Magharibi 'B';
5. Mkuu wa Wilaya ya Magharibi 'A';
6. Mkuu wa Wilaya ya Mjini;
7. Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini 'A';
8. Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini 'B';
9. Mkuu wa Wilaya ya Kusini;
10. Mkuu wa Wilaya ya Kati;
11. Mkuu wa Wilaya ya Wete;
12. Mkuu wa Wilaya ya Micheweni;
13. Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake;
14. Mkuu wa Wilaya ya Mkoani. *(Makofi)*

Pia wapo Makatibu Wakuu kama ifuatavyo:-

1. Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;
2. Katibu Mkuu Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
3. Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango;
4. Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria;
5. Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji;
6. Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali;
7. Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya;
8. Katibu Mkuu Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto;
9. Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale;
10. Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati;
11. Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi;
12. Katibu Mkuu Wizara ya Biashara na Viwanda;
    Katibu Mkuu Wizara Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ;
13. Katibu Mkuu Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora;
    Katibu Mkuu Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo. *(Makofi)*

Wapo pia Viongozi wa Vyama vya Siasa nao ni kama ifuatavyo:-

1. Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu CCM;
2. Katibu Mkuu wa *CUF;*
3. Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania;
4. Katibu Mkuu Demokrasia Makini;

5. Naibu Katibu Mkuu *TLP;*
6. Naibu Katibu Mkuu *UDP;*
7. Naibu Katibu Mkuu *TADEA*;
8. Naibu Katibu Mkuu *UMD;*
9. Naibu Katibu Mkuu *NLD;*
10. Naibu Katibu Mkuu CCK;
11. Naibu Katibu Mkuu SAU;
12. Katibu Mkuu *ADC;*
13. Naibu Katibu Mkuu *NRA;*
14. Naibu Katibu Mkuu *DP;*
15. Naibu wa *UPDP;*
16. Naibu wa CHADEMA;
17. Naibu wa CHAUMA;
18. Naibu wa *NCCR*- Mageuzi;
19. Naima Salum Hamad *UDP* (Mgombea Uspika); *(Makofi)*

Pia wapo Viongozi wa Dini nao ni :-

1. Mufti Mkuu wa Zanzibar;
2. Kadhi Mkuu wa Zanzibar;
3. Katibu wa Mufti;
4. Askofu wa Kanisa la Anglican – Dayosisi ya Zanzibar Mkunazini;
5. Askofu wa Kanisa Katoliki - Jimbo la Zanzibar Minara Miwili. *(Makofi)*

Kuna wangeni wa Katibu wa Baraza la Wawakilishi nao ni:-

1. Mhe. Dkt. Abdallah Hassan Makame – Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki

Pia tuna Taasisi ambazo zimefika ni:-

2. *Bank of Tanzania* (*BOT*);
3. *PBZ;*
4. *NMB;*
5. *CRDB;*
6. *NBC. (Makofi)*

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi baada ya kutambua wageni wote ambao wamefika kwa ajili ya kusikiliza hotuba yako, sasa kwa heshima na taadhima nachukua nafasi hii kukukaribisha ili sasa tupate kukusikiliza. *(Makofi)*

## HOTUBA YA MHE. RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KATIKA UZINDUZI WA BARAZA JIPYA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

**Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe**.** Zubeir Ali Maulid, Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdalla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Omar Othman Makungu, Jaji Mkuu wa Zanzibar. Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Waheshimiwa

Mabalozi Wadogo mliopo hapa Zanzibar, Wawakilishi wa Mashirika mbali mbali ya Kimataifa mliopo, Waheshimiwa Viongozi mbali mbali wa Serikali na Vyama vya Siasa, ndugu wageni waalikwa, ndugu wanahabari mabibi na mabwana *Assalam Alaykum.*

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia uhai na afya njema, na kutuwezesha kukutana katika siku hii ambayo ina nafasi yake katika historia ya nchi yetu. Leo tumekutana hapa kuzindua rasmi Baraza la Kumi la Wawakilishi la Zanzibar ambalo limeambatana na kuanza kwa Awamu ya Nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kabla sijaendelea na hotuba yangu, nachukua fursa hii kutoa salam za pole kwa Uongozi na Wanachama wa Chama cha *ACT* Wazalendo, familia pamoja na ndugu wa marehemu Abubakar Khamis Bakary aliyekuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Mteule wa Jimbo la Pandani. Tutamkumbuka marehemu Abubakar kwa mchango mkubwa alioutoa kwa maendeleo ya Zanzibar katika nyadhifa zake mbali mbali za uongozi alizowahi kushika likiwemo suala la Maridhiano ya Kisiasa yenye lengo la kuleta Umoja wa Kitaifa hapa Zanzibar. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amsamehe makosa yake na ailaze roho yake mahali pema peponi. Amin. Aidha, tunamuomba Mwenyezi Mungu awape wafiwa wote subira katika kipindi hiki cha msiba wa mwenzetu huyo.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu kwanza nitoe pongezi zangu nyingi kwako kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi. Kuchaguliwa kwako kwa kura zote ni kielelezo cha imani kubwa waliyonayo Waheshimiwa Wajumbe. Umefanya kazi nzuri kwa kuliongoza Baraza la Tisa na ndio sababu umeaminiwa kuliongoza Baraza la Kumi. Wahenga wamesema 'Chanda chema huvikwa pete'. Ahadi yangu kwako ni kukupa kila aina ya ushirikiano utakaohitaji katika kutekeleza majukumu yako.

Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nane unayoiongoza yatategemea sana ufanisi wa Baraza la Wawakilishi. Chombo hiki ndio chombo cha uwakilishi wa wananchi. Ndio chombo kilichopewa dhamana ya kusimamia serikali. Mimi naamini kuwa Baraza la Wawakilishi imara huzaa serikali imara. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pamoja na salamu za pongezi kwako, naomba uniruhusu nimpongeze Mhe. Mgeni Hassan Juma kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Nakutakieni kila la kheri katika kutekeleza majukumu yenu na katika kutimiza dhima kubwa mliyopewa. Kwa hakika kuchaguliwa kwenu kwa kura zote kuongoza mhimili huu wa dola kumeashiria imani waliyonayo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kwenu, kutokana na hekima na busara, uadilifu, taaluma na uzoefu mlionao. Hongereni sana. Sisi katika serikali tupo tayari kushirikiana na nyinyi katika kuijenga nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niwapongeze pia Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa kuchaguliwa na wananchi kuwawakilisha katika Baraza hili tukufu. Mimi na nyinyi tumeshirikiana katika uchaguzi na kufanya kampeni. Tumewasikia wananchi wetu ni matarajio yao kwetu. Kote nilikopita mimi na bila ya shaka nyinyi mmekutana na kiu kubwa za wananchi wetu ya kuitaka kufanya maisha yao kuwa bora zaidi. Wametuchagua kwa sababu tumeahidi kutimiza matarajio yao. Heshima yetu itatokana na sisi kutimiza matarajio hayo.

Aidha, heshima yetu itatokana na sisi kutimiza ahadi zetu. Maana sio tu kwamba ahadi ni deni, bali pia kutimiza ahadi ni kulinda heshima. Niwatakie kila la heri katika kutimiza

majukumu yenu. Niwahakikishie dhamira yangu na ya serikali nitakayoiunda ni kushirikiana na nyinyi katika kufanikisha kutimiza matarajio ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika Baraza hili la Kumi mbali na nyinyi Wawakilishi wa kuchaguliwa, kwa Mamlaka niliyopewa na Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 toleo la 2010, nimefanya uteuzi pamoja na wengine kwa Mhe. Hemed Suleiman Abdalla kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Makamu wa Pili wa Rais, pamoja na Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ninayo furaha kumtambulisha kwenu Mhe. Hemed Suleiman Abdalla kuwa Makamu wangu wa Pili na Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi. Ni kiongozi kijana mwenye ari na nguvu nyingi za kuwatumikia Wazanzibari. Ni kiongozi msikivu mwenye huruma na mchapa kazi hodari. Nakuombeni sana mumpe ushirikiano wenu. *(Makofi)*

Pamoja naye ninayo furaha kumtambulisha kwenu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Mwinyi Talib Haji, ni kiongozi mnyenyekevu, muungwana na ni mtu makini sana. Ni msomi mzuri aliyebobea katika masuala ya sheria. Tumempa jukumu hili atusaidie ndani ya Serikali na katika Baraza lako tukufu katika kutekeleza majukumu yake ya utungaji wa sheria. Nakuombeni na yeye mumpe ushirikiano wenu wote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kadhalika nakipongeza Chama changu cha Mapinduzi kwa kupata ushindi mkubwa wa asilimia 76.2 kwa nafasi ya Urais wa Zanzibar na asilimia 92 ya Majimbo kwa nafasi za Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi, na asilimia 93.6 kwa nafasi za Madiwani. Huu ni ushindi mkubwa na wa kihistoria ambao haujapata kutokea katika chaguzi zilizopita Zanzibar katika mfumo wa vyama vingi. Kwa hakika kura nyingi tulizopigiwa na wananchi ni ishara ya matumaini makubwa waliyonayo kwa uongozi mpya. Ushindi huu mkubwa tulioupata ni ishara ya imani kubwa waliyonayo wananchi kwa chama chetu na kwangu mimi binafsi. Hivyo, ni wajibu wetu sasa kukidhi matarajio ya wengi ambalo ndilo jukumu kubwa lililo mbele yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, natoa shukrani kwa viongozi wa vyama vyote vya siasa vilivyoshiriki katika uchaguzi, kuyapokea matokeo na kuheshimu uamuzi wa wananchi katika uchaguzi huo. Napenda nisisitize kuwa, tuyaheshimu maridhiano na matakwa ya kikatiba ya kushirikiana na vyama vyengine vya kisiasa katika kuendesha serikali na kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Napenda kuvihakikishia tena vyama hivyo kwamba nipo tayari kuyatekeleza maridhiano kama Katiba ya Zanzibar inavyoelekeza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimekuja Barazani leo hii kutimiza takwa la Katiba yetu la kutaka kulizindua rasmi Baraza la Wawakilishi. Ninayo furaha na fahari kubwa kutekeleza takwa hilo. Hivyo, napenda kuitumia fursa hii kuzungumza na nyinyi mambo muhimu yanayohusu ustawi wa nchi yetu, watu wetu na dhima ya Serikali ya Awamu ya Nane. Lengo langu ni tuweze kufahamiana juu ya tulipo, tunapotaka kwenda na namna ambavyo sisi katika serikali tumejipanga kutafsiri na kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 hadi 2025, ambayo Chama cha Mapinduzi kinachounda serikali kimetuelekeza kuitekeleza. Nafanya hivyo, ili wenzetu katika Baraza mtufahamu na kuona namna bora ya kutusaidia kufanikisha azma hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninaposimama mbele yenu leo ninafarijika na mambo matatu makubwa. Kwanza mimi ni Rais wa Awamu ya Nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kabla yangu kumekuwepo na Marais saba na wote hawa wamefanya kazi kubwa ya kuitoa Zanzibar ilipokuwa na kuifikisha ilipo leo ikiwa ni mafanikio makubwa. Kutangulia kwao na kazi

nzuri waliyoifanya kunanifanya mimi kuanza mahali pazuri zaidi kuliko pale walipopokea wao. Kipekee nimshukuru sana na nashukuru sana kuipokea nchi kutoka kwa Rais wa Awamu ya Saba na mzee wangu Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein amefanya kazi kubwa sana yenye kustahili pongezi zetu nyingi. Jukumu liliopo mbele yetu ni kumalizia pale ambapo hakukamilisha, kuyaendeleza mazuri aliyoyaacha na kufanya mengine mapya ya kuipeleka nchi yetu mbele. *(Makofi)*

Pili, nimepata bahati na heshima kubwa ya kuwaongoza wananchi wa Zanzibar ambao asilimia 93 kati yao wamezaliwa baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Mwaka 1964 na Muungano wetu wa Mwaka 1964. Najisikia fahari kuwa Rais wa kwanza kuiongoza Zanzibar ambaye amezaliwa baada ya matukio hayo mawili muhimu katika historia yetu. Hii kwangu ina maana kubwa sana nayo ni kuyatafsiri upya Mapinduzi yetu na Muungano wetu katika kizazi kipya. Tafsiri si nyengine bali ni kuijenga Zanzibar mpya kwa kufanya mapinduzi mapya ambayo ni Mapinduzi ya Kiuchumi. *(Makofi)*

Ikumbukwe pia kuwa lengo la Mapinduzi halikuwa tu kuondosha usultani bali kuleta uhuru na ustawi kwa Wananchi wa Zanzibar. Hilo la kwanza la Uhuru tumefanikiwa, hilo la pili la ustawi bado tunayo safari ndefu. Ni matamanio yangu kuyadumisha Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuyatafsiri katika muktadha na mahitaji ya sasa ambayo ni ukombozi wa kiuchumi. Hiyo, ndio itakuwa tafsiri yangu na ya serikali nitakayoiunda ya ile kauli mbiu yetu tukufu, Mapinduzi Daima. *(Makofi)*

Tatu, kote nilikopita wakati wa kuomba ridhaa kwa wananchi wa Zanzibar nimekutana na ari, shauku na utayari wa hali ya juu ya wake kwa waume, vijana kwa wazee, wakulima kwa wavuvi, wafanyabiashara na wafanyakazi pamoja na makundi yote kwa kuyapokea Mapinduzi mapya ya Kiuchumi na kuijenga Zanzibar mpya. Wananchi wetu wamechoshwa na siasa za uhasama, kuhubiri chuki na visasi ambazo hazibadilishi hali ya maisha yao kuwa bora zaidi. Wanataka matunda ya Mapinduzi na sio simulizi za Mapinduzi na Muungano. Wanachotaka ni kufaidika na matunda ya Mapinduzi kwa usawa bila upendeleo wala ubaguzi. Mimi ninakubaliana nao. Na mimi nimewaahidi kwamba, Yajayo ni Neema Tupu. *(Makofi)*

Kwa mnasaba huu, nimedhamiria kuwaunganisha wananchi wote kuwa wamoja bila ya kujali rangi, asili, jinsia, imani za kidini au itikadi za kisiasa. Jambo ambalo tayari nimeanza kulitekeleza katika uteuzi wa viongozi ninaoendelea kuufanya. Ifahamike kwamba uteuzi wa viongozi na watendaji katika serikali yangu utazingatia uwezo wa mtu kitaaluma, uwajibikaji na uaminifu. Narudia, uteuzi wa watendaji katika serikali yangu utazingatia uwezo wa mtu kitaaluma, uwajibikaji na uaminifu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika kuijenga Zanzibar mpya, moja ya ahadi yangu kubwa niliyoitoa kwa wananchi na ambayo imeelekezwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ni kujenga uchumi wa kisasa, Uchumi wa Buluu *(Blue Economy).* Uchumi wa Buluu ama Uchumi wa Bahari unafungamanisha kwa pamoja sekta za uvuvi, ufugaji samaki, ujenzi wa viwanda vya kusindika samaki, ukulima wa mwani, uchimbaji wa mafuta na gesi, matumizi bora ya rasilimali mbali mbali za bahari, pamoja na shughuli za utalii wa fukwe na michezo ya baharini. Zanzibar hatukujaaliwa ardhi kubwa, nchi yetu ni visiwa. Idadi ya watu wetu imeongezeka mara tano katika kipindi cha miaka 56. Mwaka 1964 Wazanzibari tulikuwa laki tatu, leo tupo takribani milioni na laki sita, wakati huo huo visiwa vyetu havipanuki wala kuongezeka, ndio kusema ardhi yetu inazidi kuwa finyu mwaka hadi mwaka.

Ahueni tuliyonayo, tulikuwa na eneo kubwa la bahari. Hivyo, sisi Wazanzibari hatuna budi tuigeuze bahari hii kuwa ndio shamba letu. Huko ndiko fursa na ajira za Zanzibar mpya zilipo. Huo ndio msingi wa dhana nzima ya Uchumi wa Buluu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, uvuvi ndio eneo ambalo hatujalitumia vya kutosha na linaweza kutuletea manufaa mengi. Serikali itaweka mkazo juu ya kuendeleza uvuvi wa bahari kuu kwa kununua vyombo vitakavyoweza kutumika kwa aina hiyo ya uvuvi. Nitazitekeleza ahadi nilizozitoa wakati nilipokutana na wawakilishi wa wavuvi zikiwemo ahadi za kuwawezesha wavuvi kwa kuwapatia vyombo vya kisasa na mikopo kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao. Hili litakwenda sambamba na kuboresha masoko yaliyopo na kujenga masoko mapya ikiwa ni pamoja na viwanda vya usindikaji samaki kwa ajili ya kuuza ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Vile vile, katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba hasa yale yenye bahari zenye mikoko na zenye mazingira mazuri, tumedhamiria kuimarisha shughuli za ufugaji wa samaki kama nilivyowaahidi katika kampeni. Serikali itazalisha na kusambaza kwa wananchi vifaranga vya samaki milioni kumi kila mwaka kwa watakaojishughulisha na ufugaji wa samaki.

Kwa upande wa zao la Mwani tutaongeza uzalishaji kwa kuwawezesha wakulima wa zao hilo. Kama nilivyowaahidi wakati wa kampeni tutawapatia vifaa na mikopo nafuu wakulima wa mwani, tutajenga viwanda vya kusarifu mwani, tutawatafutia masoko mapya ili zao hilo liwe na bei kubwa zaidi itakayosaidia kuinua hali ya maisha na kipato chao hasa kwa akina mama. Ninawataka Wajumbe wa Baraza hili la Kumi, muwe mstari wa mbele kuisimamia serikali na kuishauri juu ya namna bora ya kutekeleza azma yetu hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Serikali ya Awamu ya Nane itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kukuza na kuimarisha Sekta ya Utalii ambayo hivi sasa ndio mhimili mkuu wa uchumi wetu. Tutashirikiana kuitangaza Zanzibar katika masoko ya asili na masoko mapya. Kuendelea na ujenzi wa hoteli za daraja la juu na miundombinu mingine. Kulinda na kuhifadhi vivutio vya utalii vilivyopo pamoja na kuanzisha vivutio vyengine vipya. Ninapata matumaini makubwa kuona kwamba licha ya kuwepo kwa changamoto kadhaa zilizosababishwa na maradhi ya *Covid 19*, bado kuna mashirika mengi ya ndege na yale yanayojishughulisha na biashara ya utalii yanataka kufanya safari za kuja Zanzibar kwa ajili ya kuleta wageni. Tumepata taarifa ya ongezeko la wageni katika siku za karibuni. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuendelea kuimarika kwa Sekta ya Utalii hivi sasa kumenipa matumaini kwamba tutaweza kuyafikia malengo yaliyowekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya kuongeza idadi ya wageni wanayoitembelea Zanzibar kutoka 538,264 mwaka 2019 hadi kufikia watalii 850,000 mwaka 2025.

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu, tuna kazi kubwa ya kushajihisha na kuendeleza mpango wa utalii kwa wote yaani *Tourism for All*, ulioanzishwa na awamu iliyopita ili manufaa ya sekta hii yamguse kila mwanachi kama ilivyokusudiwa. Nimeahidi na nitatekeleza ahadi ya kuongeza utalii katika kisiwa cha Pemba. Nina azma ya kukifanya Kisiwa cha Pemba kuwa Eneo Maalum la Uwekezaji, yaani *Strategic Investment Area* kwa kutoa vivutio mahsusi kwa wawekezaji ili maendeleo ya Unguja yaende sambamba na maendeleo ya Pemba. *(Makofi)*

Serikali ninayoiongoza itahakikisha kwamba juhudi zetu za kukuza utalii zinakwenda sambamba na utekelezaji wa mipango yetu ya kuelimisha jamii umuhimu wa kulinda na

kutangaza utamaduni wetu, kuyathamini mambo ya kale, pamoja na kuendeleza historia ya Urithi wa Zanzibar ukiwemo Mji Mkongwe ambao umepata umaarufu mkubwa hivi sasa duniani kote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Sekta ya Mafuta na Gesi ni miongoni mwa maeneo makuu ya Uchumi wa Buluu. Serikali ya Awamu ya Nane itaendeleza juhudi za kushughulikia sekta hii. Tarehe 23 Oktoba, 2020 Mhe. Rais Mstaafu wa Awamu ya Saba, Dkt. Ali Mohamed Shein alitoa taarifa maalum kwa waandishi wa habari kuhusu matokeo ya awali ya tafiti zilizofanywa katika utafutaji na uendelezaji wa rasilimali hiyo. Ufupisho wa taarifa iliyotolewa ni kwamba, tafiti zilizofanywa zimeonesha uwezekano mkubwa wa kuwepo miamba yenye kuhifadhi rasilimali za mafuta na gesi asilia. Utafiti huo umeonesha kuwepo kwa maumbile ya miamba yenye uwezo wa kuhifadhi rasilimali ya gesi asilia yenye ujazo wa futi trilioni 3.8, matokeo haya ya utafiti yanathibitisha ile Kauli Mbiu yetu kwamba "Yajayo ni Neema Tupu".

Tumeshafikia makubaliano ya kindugu baina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulitoa suala la mafuta na gesi katika mambo ya Muungano. Na hivi sasa, sheria mbali mbali zimeshatungwa za kusimamia sekta hiyo, kwa hivyo Zanzibar itanufaika moja kwa moja na mapato yote yanayotokana na rasilimali hiyo wakati wowote kazi ya uchimbaji itakapoanza. Kwa hivyo, Serikali ya Awamu ya Nane itaziimarisha na kuzijengea uwezo wa kitaalamu na nguvu kazi Kampuni ya Mafuta Zanzibar *(ZPDC)* na Mamlaka ya Usimamizi wa Mafuta na Gesi *(ZPRA)* ili ziweze kuiongoza sekta hii muhimu. Vile vile, tutaendelea kushirikiana na kampuni mbali mbali zenye dhamira njema ya kuwekeza katika nchi yetu kwenye sekta hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Serikali ya Awamu ya Nane ina malengo ya kujenga bandari kubwa katika maeneo ya Mangapwani. Bandari hiyo ya kisasa itakuwa kubwa yenye sehemu kadhaa za kutolea huduma, zikiwemo sehemu za kuhudumia meli zitakazobeba mafuta na gesi, chelezo kwa ajili ya matengenezo ya meli, eneo la kuhudumia meli zinazobeba mizigo na kontena, bandari ya uvuvi na bandari ya meli za kitalii. Mhe. Spika, Uchumi wa Buluu haukamiliki bila ya kuwepo kwa bandari za kisasa zenye ufanisi wa hali ya juu.

Kwa upande wa bandari yamekuwepo malalamiko wa wafanyabiashara kuhusu kucheleweshwa mizigo yao bandarini na msongamano wa makontena katika Bandari ya Malindi. Vitendo vya rushwa na kukosa uwajibikaji kwa baadhi ya watumishi wa bandari. Kwa kutambua umuhimu wa bandari kwa Zanzibar sikukawia kuanza na jambo hili mara tu baada ya kuapishwa kwangu.

Tarehe 3 Novemba, 2020 niliamua kutembelea Bandari ya Malindi ili kuweza kufahamu kwa kina malalamiko ya wafanyabiashara na wananchi kuhusiana na utendaji kazi na utoaji wa huduma usioridhisha unaofanywa na wafanyakazi katika bandari yetu hii. Bandari ni lango kuu la biashara duniani, kwa hivyo kukosekana kwa ufanisi unaopelekea usumbufu kwa wafanyabiashara katika bandari yetu kuu ya Malindi unazorotesha kasi ya ukuaji wa uchumi wetu kwa sababu wafanyabiashara hao hulazimika kutumia bandari nyengine hasa za Dar-es-Salaam na Mombasa.

Mhe. Spika, katika Uzinduzi wa Baraza hili la Kumi la Wawakilishi nataka niwajulishe viongozi na wafanyakazi wote katika bandari zetu kuu za Unguja na Pemba, pamoja na viwanja vya ndege kwamba nitakuwa nikifuatilia kwa karibu utendaji wa taasisi hizo. Nieleweke bayana kwamba, sijaridhishwa na uendeshwaji wa shughuli za bandari na viwanja vyetu vya ndege katika maeneo yote hasa utoaji wa huduma, uendeshaji, ukusanyaji na

udhibiti wa mapato, kiwango cha faida kinachopelekwa serikalini kila mwaka pamoja na mipango ya matumizi ya fedha za maendeleo. *(Makofi)*

Nitahakikisha kwamba wafanyakazi wa bandarini na viwanja vya ndege ni wale wanaopenda kazi ya kuwatumikia watu na sio wale wenye malengo binafsi ya kujinufaisha. Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa tayari tumeshaanza kuzifanyia kazi changamoto hizo ikiwemo kujaza nafasi ya Mtendaji Mkuu katika Mamlaka ya Bandari. *(Makofi)*

Hili ni eneo ambalo nitalisimamia kwa nguvu zangu zote, maana ni eneo lenye fursa ya kutupa mapato mengi ya kuindeleza Zanzibar yetu. Vile vile, tumedhamiria kuimarisha Bandari za Wete na Shumba Mjini. Kadhalika tutaimarisha Bandari ya Mkoani ili iweze kuhudumia meli kubwa kutoka nje moja kwa moja kwa lengo la kunyanyua uchumi na biashara kwa Kisiwa cha Pemba. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Serikali ya Awamu ya Nane itaendeleza dhamira njema ya kukuza Sekta za Biashara na Viwanda hapa Zanzibar, ili kuwaletea wananchi wake maendeleo zaidi ya kiuchumi. Katika kipindi changu cha uongozi nitahakikisha kwamba Sekta Binafsi zinaashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mipango na mikakati iliyopo ya ujenzi wa viwanda vidogo vidogo, vya kati na vikubwa vyenye kuzalisha bidhaa bora zenye viwango na vyenye kuhimili ushindani wa soko. Nitahakikisha tunatekeleza ahadi niliyoitoa katika wilaya mbali mbali za Unguja na Pemba ya kujenga viwanda mbali mbali ikiwemo viwanda vya kusarifu mwani, kusindika samaki na mazao mengine ili kuyaongezea thamani.

Serikali itahakikisha inavilinda viwanda dhidi ya ushindani usio wa haki wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi ambazo hazilipiwi kodi stahiki. Serikali inatambua ya kwamba hii ndio njia ya uhakika ya kutengeneza ajira, kutoa soko kwa malighafi za ndani na kuongeza pato la serikali linalotokana na kodi stahiki zitakazolipwa na viwanda hivyo.

Mhe. Spika, ili tuweze kutekeleza kwa ufanisi ujenzi wa uchumi mpya ni lazima tuongeze uwezo wetu wa kukusanya kodi. Serikali ya Awamu ya Nane itaongeza nguvu katika upanuzi wa wigo wa kodi na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa kodi. Tutahakikisha kwamba kila mtu anayestahili kulipa kodi analipa kodi stahiki, aidha tutahakikisha kwamba kila senti inayoongezeka katika mapato ya serikali inaelekezwa katika kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi. Tutaziba mianya ya upotevu wa fedha za serikali ambayo inaipunguzia serikali uwezo wake wa kuwahudumia wananchi.

Mhe. Spika, naamini kwamba ili kuweza kutekeleza kwa ufanisi dhamira yetu ya kufanya mageuzi ya kiuchumi ni lazima pawe na ushirikiano mzuri na kuaminiana kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Wakati wa kampeni za uchaguzi nilikutana na viongozi waliowakilisha sekta binafsi kwa lengo la kujadiliana, kubuni na kutafuta njia bora za kuimarisha uhusiano na ushirikiano katika kujenga nchi yetu.

Serikali ya Awamu ya Nane itaweka mazingiza mazuri ya uwekezaji na uendeshaji wa biashara ili sekta binafsi iwe na mchango mkubwa zaidi katika kukuza ajira na katika pato la taifa. Ushirikiano na umoja wetu ndio utakaotuwezesha kutekeleza miradi yenye tija ikiwemo uendelezaji wa viwanda, utalii na uchumi wa buluu kwa ujumla wake. Ili kufanikisha azma hii serikali itaweka mifumo rafiki kwa sekta binafsi kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Kadhalika, serikali itaweka mazingira rafiki kwa wana-*Diaspora* kuja kuwekeza nyumbani kwa lengo la kuleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi tunayoyakusudia kuyafanya. Nataka

niwahakikishie wadau wa sekta binafsi kwamba serikali yangu haitakuwa kikwazo kwa sekta binafsi bali tutakuwa wadau wezeshi. Kwa mnasaba huu, sitokubaliana na visingizio vya aina yoyote na uzembe wa watendaji viweze kukwamisha azma yangu hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mapinduzi makubwa ya uchumi tunayoyatarajia yanahitaji kuwa na viwanja vya ndege vya kisasa vyenye ubora wa kimataifa. Tutaendeleza jitihada zilizofanywa za kuimarisha kiwanja cha ndege cha Abeid Amani Karume hasa baada ya ujenzi wa jengo la *Terminal III*. Hatua hiyo, sio tu umeiongezea hadhi na haiba ya uwanja huo bali pia itawezesha kuzihudumia ndege kubwa zaidi pamoja na idadi kubwa zaidi ya abiria, mizigo na watalii wanaoitembelea Zanzibar. Aidha, tunathamini jitihada zilizofanywa katika kuimarisha miundombinu ya Uwanja wa Ndege wa Pemba ikiwemo kuongeza majengo ya kutolea huduma pamoja na kuwekwa taa za kuongozea ndege. Tutaendelea na juhudi za kuimarisha viwanja hivyo pamoja na huduma zinazotolewa, ili viwe na mchango zaidi katika kuongeza ukusanyaji wa mapato na kukuza soko la ajira.

Mhe. Spika, ujenzi wa barabara bora za kisasa ni muhimu katika kufikia mapinduzi ya uchumi mkubwa na wa kisasa tunaotarajia kuujenga. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo nimeahidi kuendeleza kazi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa zaidi ya kilomita 197.6 Unguja na Pemba. Miongoni mwa barabara zitakazojengwa hapa Unguja ni Tunguu – Jumbi kilomita 9.3, Jozani – Charawe - Ukongoroni – Bwejuu kilomita 23.3, Fumba – Kisauni kilomita 12, Kizimbani – Kiboje kilomita 7.2, Kichwele – Pangeni kilomita 4.8 nyengine ni barabara ya Umbuji – Uroa kilomita 6.9, Mkwajuni – Kijini kilomita 9.4 na Tunguu – Makunduchi kilomita 48.

Vile vile, kwa kuzingatia usumbufu wanaopata wananchi wanaoishi vijiji vya Uzi na Ng’ambwa serikali itashughulikia ujenzi wa barabara na daraja kutoka Unguja Ukuu hadi Kisiwa cha Uzi. Kwa upande wa Pemba, tutazijenga kwa kiwango cha lami barabara ya Chake Chake – Wete kilomita 22.1, Mkoani – Chake Chake kupitia Chanjaani kilomita 29 na barabara ya Finya ya Kicha kilomita 8.8. Vile vile, tutazitengeneza barabara za ndani za Unguja na Pemba ili zipitike kwa urahisi wakati wote.

Mhe. Spika, uchumi mkubwa wa kisasa tunaoukusudia unahitaji kupatikana kwa nishati ya umeme ya kutosha na yenye uhakika. Dhamira yetu ya kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya viwanda inahitaji kuwa na umeme wa kiwango kikubwa. Kwa upande wa Unguja mahitaji ya umeme hivi sasa yameshafikia megawati 80 ambapo laini mpya ya umeme tulionao ina uwezo wa kuchukua megawati 100 na ile ya zamani ina uwezo wa kuchukua megawati 40 tu. Kwa mantiki hii, baada ya kipindi kifupi kijacho kiwango cha umeme tulichonacho kitakuwa ni changamoto katika kufikia dhamira yetu ya kujenga uchumi mpya wa kisasa. Hali hii inatulazimisha kuanza kuendeleza suala la kutafuta vyanzo vipya vya umeme ikiwemo nishati mbadala ili nchi yetu iwe na umeme wa uhakika.

Mhe. Spika, sambamba na miongozo ya Ilani ya Uchaguzi Serikali ya Awamu ya Nane itaweka mkazo kubwa katika kuimarisha sekta ya huduma za fedha kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na uendeshaji wa shughuli za kibenki, mashirika ya bima na taasisi nyengine za fedha. Dhamira yetu ni kuona kwamba huduma za fedha zinazotolewa na taasisi binafsi na serikali zinakidhi viwango na mahitaji halisi ya wawekezaji, watalii, wageni wanaotutembelea pamoja na wananchi kwa ujumla. Serikali itasimamia utendaji wa mashirika yake kwa lengo la kuhakikisha kwamba taasisi hizo zinatoa huduma bora zenye kuaminika kwa wateja wote.

Mhe. Spika, matumizi bora ya teknolojia ni msingi muhimu katika juhudi zetu za kuendeleza viwanda, biashara, utalii, huduma za fedha na shughuli mbali mbali za kijamii. Kwa msingi huo, Serikali ya Awamu ya Nane ina lengo la kuendesha shughuli zake katika mifumo ya kisasa ya kidijitali. Tutaweka mifumo ya kidijitali katika ukusanyaji wa kodi za serikali, manunuzi ya umma na uendeshaji wa serikali kwa ujumla. Aidha, serikali itaimarisha mitaala na masomo ya sayansi katika skuli, vituo na taasisi za ufundi pamoja na vyuo vikuu, ili kuwaandaa vizuri vijana wetu na hatimae kuweza kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia katika sekta zote.

Mhe. Spika, Serikali ya Awamu ya Nane itaendeleza mipango na mikakati iliyoanzishwa na Serikali ya Awamu ya Saba katika kuendeleza sekta ya kilimo, ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inajitosheleza kwa mahitaji ya chakula. Tutaendeleza Mpango Mkuu wa Umwagiliaji Maji Zanzibar *(Zanzibar Irrigation Master Plan)* ambao umebainisha kuwa zipo hekta 8,521 zinazofaa kujengwa miundombinu ya umwagiliaji maji. Hivi sasa jumla ya hekta 2,527 tayari zinaendelea kujengwa miundombinu ya umwagiliaji kutoka hekta 700 za mwaka 2010. Ujenzi huo unaendelezwa katika mabonde ya Cheju, Kilombero, Chaani, Kibokwa, Kinyasini kwa Unguja na Mlemele na Kwararani kwa upande wa Pemba.

Halikadhalika, serikali itahakikisha inaendeleza huduma za ugani kwa kuajiri wataalam wa kutosha na kutoa vifaa vinavyohitajika. Kadhalika tutaendeleza kuhimiza kilimo cha kisasa katika uzalishaji wa mazao mengine ya chakula kwa kuwawezesha vijana kuendeleza kilimo cha ujenzi wa vitalu nyumba *(green house)* na matumizi ya mbegu bora za kilimo. Vile vile, tutaweka mkazo katika kununua pembejeo za kilimo, dawa za kuulia magugu pamoja na kuwapatia wakulima huduma bora za matrekta.

Watu wengi duniani hivi sasa wanapendelea kula vyakula vinavyotokana na kilimo hai *(organic farming)* kutokana na ladha ya asili ya vyakula hivyo pamoja na uwezekano wa kuwa vinapunguza athari za kemikali. Ni jambo muhimu kwa taasisi itakayohusika na kilimo kulifanyia utafiti suala la kuendeleza kilimo hai nchini mwetu na upatikanaji wa masoko ya mazao yanayopatikana kutokana na kilimo hicho.

Mhe. Spika, kwa kutambua umuhimu wa zao la karafuu na uhusiano wake katika historia na maendeleo ya kiuchumi ya Zanzibar, Serikali ya Awamu ya Nane itaendeleza juhudi zilizopo za kuliimarisha zao hilo kwa kutoa mikopo na kuwatafutia masoko wakulima. Kadhalika, kutokana na tatizo kubwa la uhaba wa nazi unaopelekea kupanda bei ya zao hilo kila uchao serikali itaimarisha upandaji wa miche ya minazi, ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo. Serikali itasimamia na kuendeleza Programu ya Kufufua Zao la Minazi iliyoanzishwa mwaka 2019 lengo likiwa ni kuotesha miche ya minazi milioni moja na laki mbili Unguja, minazi laki saba na ishirini na Pemba minazi laki nne na thamanini ambapo asilimia 17 itakuwa ni minazi ya madafu na asilimia 83 itakuwa ni minazi yetu ya asili yaani *East African Coconut*.

Mhe. Spika, Serikali ya Awamu ya Nane itaweka mkazo katika kuendeleza shughuli za ufugaji wa njia za kisasa, ili sekta hiyo iwe na tija zaidi kwa wakulima na kuongeza mchango wake katika upatikanaji wa chakula na kuimarisha pato la taifa. Tutahakikisha patakuwa na matumizi mazuri ya pembejeo za mifugo, dawa za chanjo na kutoa elimu juu ya matumizi mazuri ya mbegu bora za mifugo. Serikali itabuni na kutekeleza mikakati madhubuti ya kukomesha wizi wa mifugo na mazao. Katika kuitekeleza mikakati hiyo tuzingatie sheria za nchi yetu na Waheshimiwa Wawakilishi muwashirikishe wananchi majimboni mwenu katika kupambana na wizi wa mifugo na mazao ya kilimo ambayo hivi sasa yamekithiri katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, ninaamini kwamba kwa juhudi za pamoja tunaweza kukomesha vitendo hivyo viovu vinavyorejesha nyuma maendeleo ya wakulima na wafugaji. Katika kuiendeleza sekta ya mifugo serikali itakaribisha wawekezaji wakubwa kwa ufugaji hasa wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa ambao wataweza kuwasaidia wafugaji wetu wadogo wadogo kuzalisha bidhaa nyengine zitokanazo na mifugo.

Mhe. Spika, utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo utazingatia sana kuwepo kwa mipango mizuri ya uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Tutahakikisha kwamba tuna matumizi mazuri ya rasilimali zisizorejesheka, utunzaji wa mali asili na misitu, fukwe pamoja na bahari. Kadhalika tutaweka mkazo katika kuhakikisha kwamba Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri zetu zinasimamia vyema jukumu lao la usafi wa miji. Nataka niweke wazi kwamba kiwango cha usafi katika miji yetu hakiridhishi, naamini kwamba Waheshimiwa Wajumbe mtaungana na mimi nikisema kwamba hakuna sababu ya kuifanya miji yetu isiwe safi. Kwa hivyo, serikali itahakikisha kwamba miji yetu inakuwa safi wakati wote kwa ajili ya kulinda afya za wananchi na kuvutia wageni wanaokuja kututembelea. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Serikali ya Awamu ya Nane itaweka kipaumbele katika kuziimarisha huduma za elimu afya na maji safi na salama kwa kuzingatia umuhimu wake kwa ustawi wa maendeleo ya jamii. Mhe. Spika, kwa kutambua umuhimu wa sekta ya elimu kama nyenzo muhimu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii, serikali itachukua hatua za kuimarisha ubora wa elimu ambayo ni haki ya msingi ya kila mwananchi. Katika kukabiliana na changamoto zinazoikabili sekta ya elimu hivi sasa serikali itaelekeza juhudi katika kuimarisha miundombinu ya elimu ikiwemo ujenzi wa skuli za kisasa na kuzikarabati skuli za zamani, kuzipatia skuli vifaa vya kufundishia na kusomea pamoja na madawati, kupitia upya mitaala ya elimu na kupunguza tatizo la walimu hasa wa masomo ya sayansi. *(Makofi)*

Kadhalika, tutaimarisha kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi katika mitihani ya taifa, kuendeleza masomo ya ufundi katika vyuo vya amali na vituo mbali mbali. Ili kufikia dhamira hiyo serikali itaongeza bajeti ya sekta ya elimu ili iweze kugharamia vyema huduma za elimu katika ngazi zote kwa kuendeleza sera ya elimu pamoja na kuongeza fursa za mikopo ya wanafunzi wanaojiunga na masomo ya elimu ya juu. Pamoja na hatua hizo, tutaimarisha maslahi ya walimu, ili kuwapa motisha ya kufundisha na tutaendeleza sera ya elimu bure kwa lengo la kuwaondolea wazazi mzigo wa kuchangia elimu ya watoto wao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nikiwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar *(SUZA)* nitahakikisha kwamba tunakiendeleza chuo hiki kwa kuanzisha programu mpya kutegemea mahitaji halisi ya nchi yetu, sambamba na kujenga majengo mapya pamoja na kukipatia vifaa vya kisasa vya kufundishia vinavyohitajika, ili kuweza kutoa elimu bora kwa wananfunzi wanaojiunga na chuo hicho. Tutaweka mkazo katika kufanya tafiti kwenye maeneo muhimu kwa kuzingatia ajenda za maendeleo ya kichumi na kijamii za nchi yetu. Tutahakikisha kwamba *SUZA* inaendelea kuwa na uhusiano mwema na Vyuo na Taasisi za Elimu ya Juu zilizopo Zanzibar na sehemu mbali mbali za dunia.

Aidha, tutaendelea kuweka mkazo maalum katika kufundisha Kiswahili ili kutekeleza dhamira yetu ya kuifanya Zanzibar kuwa chimbuko la Kiswahili Sanifu na Fasaha. Tutahakikisha kwamba wahitimu wa chuo chetu hiki katika fani zote tunazozifundisha

wanabobea kitaaluma na wanajengeka kiushindani katika soko la ajira popote wanapokwenda. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa upande wa sekta ya afya serikali itaendelea na ujenzi wa Hospitali ya Rufaa huko Binguni Wilaya ya Kati ambayo itakuwa na huduma zote za kibingwa, mpango wake upo na lazima tusimamie utekelezaji wake kwa nguvu zetu zote. Hatua hiyo itatuwezesha kupunguza na hatimae kuondoa kabisa tatizo la kupeleka wagonjwa nje ya nchi. Sambamba na juhudi hizo, tutaendelea kuimarisha miundombinu ya afya, ununuzi wa dawa na vifaa tiba, kuongeza idadi ya madaktari bingwa wa fani mbali mbali na wataalam wengine wa afya, tutaongeza bajeti ya kununulia dawa na vifaa vyengine vya huduma za afya. *(Makofi)*

Vile vile, tutaongeza nyumba za madaktari na kujenga vituo vya afya ili kuondoa usumbufu wanaopata baadhi ya wananchi kufuata vituo vya afya katika maeneo ya mbali. Aidha, tutaimarisha Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja na Hospitali za Rufaa za Makunduchi na Kivunge. Tutazijengea uwezo Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani, Hospitali ya Chake Chake na Wete pamoja na kuipandisha hadhi Hospitali ya Micheweni, lengo letu ni kuona kwamba huduma zote za kibingwa zinapatikana katika Kisiwa cha Pemba. *(Makofi)*

Katika kufikia dhamira zetu hizo tutawashajihisha wawekezaji kuwekeza katika sekta ya afya, vile vile tutaangalia uwezekano wa kuanzisha bima ya afya kwa wenye uwezo na kwa wale wasiokuwa na uwezo serikali itaendelea kuwapatia huduma za afya bure. Naomba nirudie sehemu hii vile vile tutaangalia uwezekano wa kuanzisha bima ya afya kwa wenye uwezo na kwa wale wasio na uwezo serikali itaendelea kuwapatia huduma za afya bure. *(Makofi)*

Mhe. Spika, upatikanaji wa huduma za maji bado ni changamoto katika baadhi ya maeneo ya mjini na vijijini, hali ya upatikanaji wa maji hivi sasa imefikia wastani wa asilimia 83 katika mwaka wa 2020 kwa kuzingatia kuwa maji ni uhai. Serikali ya Awamu ya Nane itamalizia kazi hii iliyobaki ya kuboresha miundombinu ya maji na kuongeza upatikanaji wake, kazi hiyo ni pamoja na kujenga matangi mapya ya kuhifadhia maji, uchimbaji wa visima vipya vya maji na kuendelea kuifanyia matengenezo miundombinu ya zamani ikiwemo kuvitengeneza visima vya zamani na kuviwekea pampu zenye nguvu zaidi. Vile vile, tutayabadilisha mabomba ya zamani na kukabiliana na tatizo la uvujaji wa maji. *(Makofi)*

Mhe. Spika, uwezeshaji wananchi kiuchumi ni miongoni mwa malengo ya Serikali ya Awamu ya Nane katika kukabiliana na tatizo la umaskini wa kipato unaosababisha na ukosefu wa ajira. Tunaelewa kuwa bado kuna changamoto zinazowakabili wananchi katika kuendesha shughuli za ujasiriamali ambazo zinahusiana na ukosefu wa mitaji, vifaa, wataalam wa kutosha wa kuendesha biashara na utafutaji wa masoko ya uhakika ya kuuzia biashara hizo.

Katika kukabiliana na changamoto hizo serikali itauimarisha Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kuwaongezea uwezo wa kutoa huduma zilizo bora kwa wananchi wengi zaidi. Kadhalika, tutawasajili wajasiriamali wote na kuwapatia vitambulisho, pia tutatoa mafunzo ya namna bora ya kuitumia mitaji na mikopo hiyo katika kupata vifaa na zana za kisasa na kuendesha shughuliza ujasiriamali kitaalam zaidi kulingana na mahitaji ya masoko ya wakati tulionao. *(Makofi)*

Aidha, tutawajengea wajasiriamali sehemu maalum za kufanyia biashara zao zitakazojengwa vizuri, ili waondokane na usumbufu wa kuhama hama huku na kule. Pamoja na jitihada hizi serikali itawawekea mfumo na utaratibu bora wa kulipa kodi mara moja tu kwa mwaka na kuondosha ile kero ya utitiri wa kodi. Katika kuhakikisha kwamba mkakati huu unaleta ufanisi tunaotarajia tutakuwa tunafuatilia kwa karibu na kufanya tathmini ya mikopo tunayoitoa kwa vikundi hivyo, ili kujiridhisha endapo inawafikia walengwa na kwamba hakuna matumizi mabaya ya fedha hizo yanayofanywa na watumishi wa serikali ambao si waaminifu. Tusitosheke tu kutoa mitaji na mikopo na baadae kuripoti takwimu za vikundi vilivyopokea mikopo hiyo na kuirejesha au kutorejesha, isipokuwa ni lazima tujue mikopo hiyo imeleta faida gani kwa wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, maendeleo, amani na utulivu ni dhana zenye maana zinazotegemeana, ili kuwe na maendeleo kunahitajika kuwe na amani na utulivu, na kwa upande mwengine amani na utulivu haiwezi kupatikana ikiwa hakuna maendeleo, ni kama uhusiano wa kuku na yai. Maendeleo katika nyanja mbali mbali za maisha ndio yanayowaletea wananchi utulivu na utulivu ndio unaoleta amani. Wananchi wanaokabiliana na dhiki za maisha hasa katika kupata huduma muhimu za kuyamudu maisha yao mwishowe hujenga hasira, hasira ambayo huzaa chuki miongoni mwao na kusababisha matendo maovu yanayopelekea kuvunjika kwa amani. Ili uwiano mzuri upatikane baina ya amani, utulivu na maendeleo ni lazima tuhakikishe kwamba serikali inayoongozwa katika misingi ya utawala bora.

Miongoni mwa mambo yanayodhoofisha misingi ya utawala bora ni vitendo vya rushwa, uzembe, kukosa uwajibikaji, kutofuata sheria na kukiukwa kwa maadili. Serikali ya Awamu ya Nane itakabiliana ipasavyo na vitendo vyote vinavyoathiri utekelezaji wa misingi ya utawala bora. Najua wananchi wanachukia sana rushwa na ufisadi na wamechoshwa na vitendo hivyo, vitendo vya rushwa na ufisadi vinawanyima haki wananchi na kuitia hasara serikali. Mimi nimewaahidi wananchi na nataka nirejee ahadi yangu kwao mbele ya Baraza lako tukufu kwamba nitapambana na rushwa na ufisadi bila ya kigugumizi wala kuoneana muhali. Ninawaomba Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi wote mniunge mkono wakati wa mapambano haya, tutashinda vita hii endapo wananchi pia watatuunga mkono, sina shaka kwa vile wao kwa wingi wao wanachukia rushwa na ufisadi watakuwa tayari kutoa ushirikiano wao katika mapambano haya. *(Makofi)*

Ni matumaini yangu pia vyombo husika katika jambo hili vitatekeleza wajibu wao. Nataka niweke wazi kuwa kiongozi yeyote nitakayemteua kwa mamlaka niliyonayo kikatiba nitamuwajibisha mara moja pindi tu nikibaini na kujiridhisha kuwa anajihusisha na vitendo vya rushwa na ufisadi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mafanikio katika utendaji wa serikali yanategemea jinsi sekta ya umma inavyotekeleza wajibu wake wa kuwatumikia wananchi kwa misingi ya uwajibikaji, usawa na haki. Utendaji katika sekta yoyote unategemea kuwepo kwa haki na utekelezaji wa wajibu, kwa maana nyengine haki na wajibu ni watoto pacha. Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba watumishi wanapata haki zao kwa mujibu wa sheria pamoja na kuwawekea mazingira mazuri ya kufanyia kazi.

Kwa upande mwengine, wafanyakazi nao wana wajibu wa kutekeleza kwa bidii na nidhamu kubwa majukumu ya kazi zao kwa mujibu wa Sheria za Utumishi kwa maslahi ya jamii na taifa kwa ujumla.

Kwa hivyo, Serikali ya Awamu ya Nane itasimamia kwa umakini sana nidhamu na uwajibikaji wa watumishi wa umma, serikali haitakuwa na muhali kwa mtendaji yeyote ambaye hatawajibika katika majukumu yake na atakayeshindwa kuwajibika aelewe kuwa atawajibishwa, uzembe na ukosefu wa nidhamu kazini huzorotesha maendeleo ya uchumi na kijamii. Kwa hivyo, tabia hii sitoivumilia hata kidogo. *(Makofi)*

Kadhalika, tunahitaji ubunifu wa kitaalam katika kufanya kazi zetu ili tuondokane na mtindo wa kufanya kazi kwa mazoea. Napenda viongozi wote nitakaowateua katika ngazi mbali mbali walizingatie jambo hili ni lazima wawe wabunifu na waweze kuishauri serikali juu ya masuala mbali mbali yanayohusu fani na utaalam wao. Serikali haitowavumilia viongozi wanaosubiri kuambiwa kutoka kwangu au serikalini nini wafanye katika kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Tutaendelea kusimamia utendaji wa Sheria ya Hifadhi ya Jamii kwa manufaa ya wanachama wote, wafanyakazi na wastaafu. Tutafungua ofisi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii katika mikoa ya Zanzibar, ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wanachama wake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, serikali itaziendeleza Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ili ziendelee kutoa huduma bora za ulinzi na usalama kwa wananchi na kutelekeza majukumu yao mengine kwa ufanisi na kwa mujibu wa sheria zinazoongoza idara zetu hizo. Tutaendeleza miradi ya ujenzi wa majengo ya ofisi, mahanga na nyumba za maafisa sambamba na kuimarisha mazingira ya kambi mbali mbali za idara zetu maalum. Vile vile, tutaendelea kuwajengea uwezo maafisa na wapiganaji kwa kuwapatia vifaa na mafunzo ya kisasa katika vyuo vya ndani na nje ya nchi. Kadhalika tutaendelea kuimarisha maslahi yao kwa kadri hali ya uchumi wetu itakavyoruhusu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mapinduzi makubwa ya uchumi tunayoyakusudia kuyafanya yatatupelekea kuwa na uchumi mpya wa kisasa ambao utaongeza fursa nyingi za ajira kwa vijana wetu. Kwa hivyo, ni wajibu wa vijana wetu kuwa tayari kufanya kazi. Serikali itawajengea uwezo kwa kuwapatia mafunzo maalum ya ufundi wa fani mbali mbali katika Vyuo vya Ufundi na Vituo vya Amali. Vile vile, vijana watawezeshwa kwa kupatiwa mitaji ili waweze kujiajiri wenyewe na kuondokana na tatizo la kutegemea ajira chache kutoka serikalini. Serikali itaandaa sera nzuri za ajira na kuwashajihisha wawekezaji kuweka kipaumbele katika kuwaajiri vijana Wazanzibari. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wazee ni hazina kubwa kwa nchi yetu na kwa kulitambua hilo serikali itaendelea kuwatunza wazee. Kwa wazee wanaoishi nyumba za Sebleni, Welezo na Limbani huduma za kuwapatia makaazi bora, chakula na matibabu zitaendelea. *(Makofi)*

Vile vile, huduma ya pencheni jamii kwa wazee waliofikia umri wa miaka sabini za zaidi zitaendelea kutolewa. Hapo baadae serikali itaangalia uwezekano wa kushusha umri na kuongeza kiwango cha pencheni inayotolewa kwa mwezi. *(Makofi)*

Kwa upande wa wanawake na watoto serikali imeazimia kuwasaidia wanawake wajane ambao tayari wameshaunda rasmi jumuiya yao. Wanawake hao watasaidiwa kwa kuwezeshwa kiuchumi na kusimamia haki zao ikiwemo mirathi. Kadhalika serikali itaendeleza juhudi zilizotangulia za kuwapatia wanawake na watoto haki zao zote za msingi ili waishi vizuri katika jamii. *(Makofi)*

Katika kulinda haki zao serikali itaendeleza mapambano ya vitendo vya udhalilishaji wa watoto na unyanyasaji wa kijinsia kwa nguvu zetu zote na kuhakikisha kwamba sheria zilizotungwa na kupitisha zinazolinda usalama na maslahi ya wanawake na watoto zinatumika ipasavyo na haki inatendeka. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama nilivyosisitizwa na kuelekezwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi serikali itaweka kipaumbele maalum katika kuwashirikisha watu wenye ulemavu kwenye shughuli mbali mbali za kiuchumi, pamoja na kuzilinda na kuziimarisha haki zao, tutawawezesha kwa kuwapatia mitaji na mafunzo mbali mbali ya ujasiriamali bila ya kuwabagua kijinsia au aina ya ulemavu walionao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo tutalishughulikia ni sanaa, burudani na michezo mambo haya matatu yana nafasi ya kipekee katika kuwaunganisha Wazanzibari, kuwatambulisha Wazanzibari duniani kwa kukuza uchumi na kutoa ajira. Muziki wa taarab, muziki wa kizazi kipya na sanaa ya filamu kupitia matamasha ya *ZIFF* na Sauti ya Busara yameitangaza sana Zanzibar na kuwa na mchango wa kipekee. Naahidi kuyalea na kuyakuza matamasha haya na mengine, ili kutangaza hazina ya utamaduni na ustaarabu wa Zanzibar ikiwa ni sehemu ya kukuza utalii, kipato na ajira. *(Makofi)*

Kwa upande wa michezo tutafanya mengi lakini kubwa sana na ambalo linanifadhaisha moyo ni kupotea kwa msisimko wa Ligi ya Soka ya Zanzibar, siku za nyuma timu za Zanzibar za *Small Simba*, Malindi, Mlandege na KMKM zilikuwa ni timu zenye sifa za kuchachafya timu za Bara na Afrika Mashariki. Tutawekeza katika michezo katika kuibua, kulea na kuendeleza vipaji vya vijana. *(Makofi)*

Hii itakwenda sambamba na kukaa na wadau wa soko kutafuta jawabu la kuamsha msisimko wa ligi yetu ya Zanzibar, azma yetu ni kuona Timu ya Taifa ya Zanzibar inakwenda mbali katika kushiriki michuano ya Afrika, ili kutumia vizuri fursa ya uwanachama wetu katika Shirikisho la Michezo la Afrika ambayo tumeipigania kwa miaka mingi. Natambua kuwa maendeleo ya michezo yanahitaji udhamini kutoka kwa wadau wa michezo naahidi kujadiliana nao, ili waweze kutoa udhamini kwa michezo yetu mbali mbali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mafanikio ya utekelezaji wa mipango na ahadi tulizozitoa hayawezi kupatikana bila ya kuendelea kuwepo kwa amani na utulivu nchini. Jukumu la kulinda na kudumisha amani tuliyonayo sio ya vyombo vya ulinzi na usalama peke yake, huo ni wajibu wa kila mmoja wetu, kuiharibu amani ni jambo jepesi na la mara moja, ila kuirudisha ni vigumu na tujifunze kwa wengine walioichezea tunu hii. Kwa hivyo, sote tuwe walinzi wa amani kwa kutambua kuwa bila ya amani hakuna maendeleo.

Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya Nane itashirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuhakikisha kuwa amani na usalama wa Watanzania na mali zao pamoja na wageni wote wanaotutembelea nchini vinadumishwa na kulindwa.

**Hitimisho**

Mhe. Spika, kabla sijamaliza hotuba yangu nawashukuru tena wananchi wa Zanzibar kwa kutupa dhima hii ya kuongoza nchi na serikali. *(Makofi)*

Tunatambua uzito wa dhamana tuliyoibeba kwa wananchi ya kuwatumikia watu wote kwa misingi ya usawa. Nakuahidini kuwa serikali nitakayoiunda itasimamia kwa uweledi na

umahiri mkubwa utekelezaji wa ahadi zote tulizozitoa wakati wa kampeni kwa ufanisi huku tukizingatia kuwa ahadi ni deni na wananchi wametuchagua kwa matumaini makubwa. *(Makofi)*

Ni matarajio yangu kuwa nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi mtazingatia wajibu wetu huu na Madiwani wetu nao watazingatia kuwa uongozi tuliopewa ni dhamana ya kuwatumikia watu na sio kwa maslahi yetu binafsi. *(Makofi)*

Kwa mara nyengine tena, nakupongeza Mhe. Spika, Naibu Spika na Wajumbe wote wa Baraza la Kumi la Wawakilishi la Zanzibar kwa heshima kubwa mliyopewa na wananchi ya kuchaguliwa kuingia katika chombo hiki muhimu cha kutunga sheria ili muwawakilishe. Matumaini yangu mtaitumia vyema fursa hii kwa lengo la kuchangia mipango ya maendeleo na kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbali mbali zinazowakabili wananchi wetu kwa kusaidiana na serikali yetu.

Namalizia hotuba yangu kwa kuvishukuru vyombo vya habari vilivyotangazia wananchi tukio hili la Uzinduzi wa Baraza. Kadhalika, nawashukuru wananchi wote wanaofuatilia uzinduzi huu kupitia vyombo vya habari. Tumuombe Mwenyezi Mungu aizidishie nchi yetu amani, umoja na mshikamano. Mola atuwezeshe kuitekeleza mipango yetu ya maendeleo kwa ufanisi.

Nakutakieni nyote kila la kheri na mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na kwa mamlaka niliyonayo ya kikatiba kama yalivyoainishwa katika ibara ya 91 kifungu kidogo cha kwanza, sasa natamka kuwa Baraza la Kumi la Wawakilishi la Zanzibar limezinduliwa rasmi leo tarehe 11 Novemba, 2020. *(Makofi)*

Mwenyezi Mungu ibariki Zanzibar, Mwenyezi Mungu ibariki Tanzania, Mwenyezi Mungu ibariki Afrika. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Waheshimiwa Wajumbe, nadhani sote tutakubaliana kwamba hotuba iliyotoka hapa ni hotuba nzuri sana na madhubuti *(strong speech)*. *(Makofi)*

Ni hotuba ambayo imegusa karibu kila sekta na inaonesha muelekeo ambao tutakwenda. Ni hotuba ambayo sasa inaturejesha kwenye yale maneno ya kwamba “Yajayo ni Neema Tupu” na “Yajayo Yanafurahisha.” *(Makofi)*

Mimi nichukue nafasi hii kwa niaba yenu kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hotuba yake ambayo ameitoa hapo lakini nisingependa kuanza kuichangia mimi. Naomba nitoe nafasi kwa mjumbe mmoja hapa alikuwa ana hoja ambayo tuisikilize hiyo hoja halafu baada ya hapo tunaweza kuamua. Ahsante sana.

**Mhe. Saada Mkuya Salum:** Mhe. Spika, nakushukuru sana na kwa niaba ya wajumbe nadhani ni muhimu sana kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar kutokana na hotuba yake ambayo pengine *commonly* tunaweza tukaiita ni *golden speech*, yaani hotuba ya dhahabu.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 21 kifungu cha 12 naomba kutoa hoja kwamba tupate muda kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuweza kujadili hotuba hii ambayo na sisi tutaweza ku-*affirm* na ku-*nailed* maeneo mazuri ambayo Mhe. Rais ameyabainisha, ili kutoa mwelekeo katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Saada Mkuya Salum. Waheshimiwa Wajumbe, hoja kama mlivyoisikia ni hoja ya kwamba tupate muda wa kuchangia hii hotuba nzuri ambayo imetolewa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Sasa naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja na Mhe. Saada Mkuya Salum wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, pamoja na kwamba tumekubaliana na hoja ya kuichangia hii hotuba jambo hilo hatutaweza kulifanya katika mkutano huu. Jambo hilo sasa tutalipanga katika kikao kinachofuata cha mkutano wa Februari, ili kukupeni nafasi na wakati huo mtakuwa mnavyo vitabu vya hiyo hotuba yenyewe na muweze kuja kuchangia humu na wananchi wasikie michango yetu ambayo pia itasaidia katika utekelezaji mzuri ambao mheshimiwa anakusudia kufanya. *(Makofi)*

Baada ya kumaliza hapo, naomba sasa nimwite Katibu kwa shughuli inayofuata.

**Katibu:** Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwako na Baraza lako Tukufu kwamba shughuli tulizozipanga hii leo zimekamilika.

**Mhe. Spika:** Ahsante. Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa shughuli zote zilizopangwa kwenye *order paper* ya leo, lakini pia kwenye mkutano wetu huu wa leo wa ufunguzi wa Baraza zimekamilika. Kwa heshima na taadhima, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ili aje atutolee hoja ya kuakhirisha Baraza. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais karibu sana. *(Makofi)*

**Mhe. Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwanza na mimi naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia afya njema na salama na tukaweza kufanya shughuli yetu hii adhimu.

Mhe. Spika, lakini kwa ruhusa yako kabla sijafanya lile ambalo limekusudiwa naomba uniruhusu dakika moja nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwanza kwa kuwa nae pamoja katika jambo hili la kihistoria, lakini la pili kwa kutoa hotuba kwenye Baraza letu Tukufu ambayo hotuba hii inatoa mwelekeo wa maendeleo na msimamo wa Serikali hii ya Awamu ya Nane itakavyokuwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunamshukuru sana sana Mhe. Rais na tunamshukuru kwa sababu wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla walikuwa wanasikia yale maneno ya kampeni "Yajayo Yanafurahisha" na "Yajayo ni Neema Tupu" lakini baada ya muelekeo wa leo naamini sana

utekelezaji wa Serikali yetu ya Awamu ya Nane kama malengo ambavyo yamekusudiwa, Mhe. Rais wananchi hawakuwa na hofu lile neno “Yajayo ni Neema tupu”. *(Makofi)*

Na mimi naamini mafanikio haya na uwajibikaji na utekelezaji ambayo yametolewa kwenye hotuba yake muhimu Mhe. Rais hatuna wasi wasi kama yale yatatekelezeka kwa vitendo.

Mhe. Spika, baada ya salamu hizo chache za shukrani sasa naomba nifanye ule wajibu wangu muhimu wa kutoa hoja ya kuakhirisha Mkutano huu wa Baraza hadi tarehe 10 Februari, 2021.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa napenda sasa nichukue nafasi na mini niwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja ya kuakhirisha Baraza wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, kwa heshima na taadhima naomba sasa niliakhirishe Baraza hili la Wawakilishi mpaka tarehe 10 Februari, 2021 saa 3:00 barabara za asubuhi. Ahsanteni sana.

*(Saa 10:00 jioni Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 10/02/2021 saa 3:00 asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA**